



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE**



**Kumb. Na HWC/L.20/24 /01**

**15/02/2022**

**TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA YA MUDA KWA NAFASI YA MKUSANYA**  
**TAARIFA KWENYE ZOEZI LA ANWANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya Muda kwa nafasi za wakusanya taarifa kwenye zoezi la Anwani za makazi katika **Kata, Vijiji na Vitongoji** vya Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze

**A: SIFA ZA WAOMBAJI**

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18-35
- ii. Awe na elimu kuanzia kidato cha Nne na kuendelea
- iii. Awe anamiliki simu janja Android yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima
- iv. Awe na barua pepe(email) na nywila (password) inayofanya kazi
- v. Awe na uwezo wa kusoma ramani za Vijiji/Mtaa/Vitongoji

**B: KAZI NA MAJUKUMU**

- i. Kugawa/kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- ii. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- iii. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa Anwani za makazi
- iv. Kutuma data kwenye mfumo wa makazi

**C: MAOMBI YAAMBATISHWE NA**

- i. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea
- ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- iii. Picha (Passport size 2)
- iv. Barua ya maombi ipitie kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa aliyepo muombaji
- v. Hakikisha unataja namba zako za simu ya Mkononi

**D: MALIPO**

Malipo yatafanyika kwa kiasi cha kazi kwa siku

**E: JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba za simu, barua pepe na ziwasilishwe ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya kupitia kwa kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa/Kitongoji aliyepo muombaji kwa anwani ifuatayo;

**Mkurugenzi Mtendaji**  
**Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze**  
**S.L.P 65**  
**CHALINZE**

**F: TAREHE YA MWISHO YA KUPOKEA MAOMBI**

Mwisho wa kupokea maombi ni Tarehe 22/02/2022 saa 9:30 Alasiri

Limetolewa na



Ramadhani Salmin Possi

**Mkurugenzi Mtendaji(W)**

**CHALINZE**

